**BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR**

**ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO**

**BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI**

**MKUTANO WA TANO**

**Kikao cha Tatu – Tarehe 21 Disemba, 2021.**
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

## I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

**Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:**

Taarifa ya Serikali kuhusu Ripoti ya Hali ya Mazingira Zanzibar.

**Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa:**

Maoni ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kuhusu Taarifa ya Serikali ya Ripoti ya Hali ya Mazingira Zanzibar.

## II. HOJA YA MJUMBE:

**Mheshimiwa Hudhaima Mbarak Tahir:**

Hoja ya Mjumbe Kuhusu kuanzishwa kwa Jumuiya ya Wawakilishi kuhusiana na Idadi ya watu na Maendeleo Zanzibar.

## III. MASWALI:

### Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:

160. MHESHIMIWA MACHANO OTHMAN SAID (Jimbo la Mfenesini) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:

Wananchi wa Zanzibar wamekuwa wakifaidika sana na miradi ya TASAF. Hata hivyo, pamoja na kufaidika huko yapo malalamiko kwamba miradi ya miundombinu kama ujenzi wa skuli, vituo vya afya na barabara imekuwa ikipelekwa katika sehemu yenye viongozi maalum.

(a) Kwa kuwa mradi wa TASAF III umemalizika mwishoni mwa mwaka uliopita Je, miradi ya elimu na afya ilifanyika katika maeneo gani kwa upande wa Unguja.

(b) Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inatarajia kupata karibu Bilioni 36 kutoka fedha za TASAF kwa kipindi hiki, Je, ni miradi gani mikubwa inatarajiwa kutekelezwa kupitia TASAF.

### Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:

190. MHESHIMIWA NASSOR SALIM ALI (Jimbo la Kikwajuni) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:

Katika Jimbo la Kikwajuni tumebahatika kupakana na bahari. Hata hivyo, ipo changamoto ya uchafuzi wa bahari hiyo hasa utupaji wa taka za plastiki ambazo zinaleta uharibifu wa mazao ya baharini.

(a) Je, kuna mkakati wowote ulioandaliwa kukabiliana na utupaji wa taka za plastiki kwenye fukwe zetu.

(b) Je, Serikali ina mpango wa kuweka siku maalum nchi nzima ya kujitolea kwa wananchi kufanya usafi kwenye fukwe zetu.

(c) Je, hatua gani zimechukuliwa kuondoa majaa yasiyo rasmi pembezoni mwa fukwe na kwenye mikoko hasa katika pwani za Kizingo, Kinazini na nyenginezo.

**Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:**

180. MHESHIMIWA SHAABAN ALI OTHMAN (Jimbo la Mpendae) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:

Rais wa awamu ya tano na sita wa Tanzania kwa nyakati tofauti wameliagiza Jeshi la Polisi pamoja na Ofisi ya DPP kuyatembelea magereza na kuzifuatilia kesi za muda mrefu ambazo zimekwama au zisizo na ushahidi wa kutosheleza, matokeo yake wapo watuhumiwa wengi sana kutoka magereza tofauti waliachiwa huru.

(a) Je, kwa magereza ya Zanzibar zoezi hilo limefanyika lini.

(b) Watuhumiwa wangapi wameweza kuachiwa huru kwa njia kama hizi na ni kutoka magereza yepi kwa Zanzibar.

**Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:**

201. MHESHIMIWA SHADYA MOH'D SULEIMAN (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:

Naipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuanzisha mfuko wa wananchi kiuchumi, lengo kuu ni kuwakwamua kinamama na hali ngumu ya maisha lakini bado kina mama hawa hawajafaidika na fedha hizi na bado fedha inayokopeshwa ni ndogo.

Je, Serikali ina mpango gani kwa kinamama hawa ambao bado wanasuwasuwa na biashara zao kutokana na mfuko mdogo wanaopata.

**Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:**

30. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Katika kusogeza huduma karibu na wananchi, Serikali imeteua Masheha katika kila shehia ndani ya majimbo. Hata hivyo, katika shehia nane zilizo ndani ya jimbo la Pandani, isipokuwa shehia moja tu ambayo wananchi hawamlalamikii na wanamtaka aendelee Sheha wao, Masheha wengine wote kwa kushirikiana na maafisa wa Mkoa wamekuwa wakilalamikiwa na wananchi.

(a) Je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha kwamba masheha wanaoteuliwa wanakubalika na Serikali pamoja na wananchi ili kuleta ufanisi.

(b) Je, ni ipi tathimini ya Serikali kuhusu utendaji kazi na utoaji huduma wa masheha wa shehia za jimbo la Pandani.

196. MHESHIMIWA NASSOR SALIM ALI (Jimbo la Kikwajuni) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Katika siku za hivi karibuni kumekuwa kukiripotiwa matukio ya watu kukabwa na kuporwa simu na vitu vyao. Inaonekana hivi sasa kumechipuka vikundi vingi mitaani vya vijana wanaotumia mihadharati ambavyo vimekuwa kero kwenye mitaa.

(a) Je, Serikali kwa nini isianzishe operesheni za mtaa kwa mtaa za saa 24, kuviondoa vikundi hivi vya vijana waovu.

(b) Je, kwanini Serikali za Mitaa kupitia masheha hazianzishi utaratibu wa kuviripoti vikundi vya vijana waovu kila muda vinapojitokeza ili kupunguza tatizo la uhalifu kwa wananchi.

**<u>Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:</u>**

6. MHESHIMIWA HASSAN HAMAD OMAR (Jimbo la Kojani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Katika miaka ya thamanini na tisini, timu ya Taifa ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kiasi fulani iliingiza wachezaji zaidi ya asilimia thelathini kutoka Zanzibar, kama vile marehemu Rifat Said, Ali Bushir ambao wote wawili wamewahi kuwa “Tanzania One”: Wengine ni Abdul Wakati Juma, Thuwain Ally, Karume Mussa, Ali Nassor Kibichwa, Duwa Said wote hawa walikuwa tishio na hatimae kutikisa soka la Zanzibar huku wakifundishwa na Kocha wazawa akina Mzee Bori na Majid Abdighani Msoma.

(a) Je, ni sababu gani za msingi zilizopelekea wachezaji wetu wa mpira wa miguu hapa Zanzibar kupoteza ubora wao na hatimae kwa kiasi kikubwa kutoingizwa kwenye timu ya Taifa ya Tanzania.

(b) Ni lini Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar itaajiri kocha wa kimataifa (Professional Coach) ili kuinua kiwango cha soka hapa nchini.

15. MHESHIMIWA MACHANO OTHMAN SAID (Jimbo la Mfenesini) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo.

Kwa muda mrefu sasa Shirika la Utangazaji la Zanzibar (ZBC) limekuwa na ushirikiano na nchi na mashirika mbali mbali kwa lengo la kuwapatia ujuzi watendaji wake, kupata vifaa na mapato.

(a) Je, Shirika hilo hadi sasa lina mikataba ya uhusiano na taasisi au nchi gani.

(b) Kwa kipindi cha miaka kumi iliyopita, Je, Shirika hili limefaidika vipi na makubaliano hayo.

**<u>Wizara ya Maji, Nishati na Madini:</u>**

72. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (Jimbo la Wawi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

Imebainika kuwa Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA) kwa upande wa Pemba inazidai taasisi za Serikali, wafanyabiashara na watu binafsi takribani Tsh. 16,007,884,152.98. Aidha, Mamlaka hii inakabiliwa na changamoto kubwa ya uhaba wa fedha.

(a) Je, ni kweli kwamba hadi kufikia mwaka wa fedha 2019/2020 ZAWA - Pemba inadai kiasi hicho cha fedha.

(b) Je, ni sababu zipi zilizopelekea uwepo wa deni hilo kubwa.

(c) Je, ZAWA ina mpango gani katika kuhakikisha kuwa deni hilo linalipwa lote.

233. MHESHIMIWA AZZA JANUAR JOSEPH (Nafasi za Wanawake) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

Kumekuwa na tatizo la kukosekana kwa maji mara kwa mara katika maeneo mengi ya Wilaya ya Chake Chake kama vile Chanjaani na Gombani.

(a) Ni lini maeneo haya yanaweza kupata maji ya uhakika.

(b) Kuna tatizo gani linalosababisha maeneo haya kukosa maji hasa tukizingatia visima vya maji vipo katika maeneo hayo.

**<u>Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:</u>**

24. MHESHIMIWA HASSAN HAMAD OMAR (Jimbo la Kojani):
Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Naipongeza Serikali kwa juhudi za kuboresha miundombinu ya mawasiliano na usafirishaji, hasa kwa kuweka mpango wa ujenzi wa barabara za vijijini kwa kiwango cha lami katika bajeti hii ya mwaka 2021/2022. Hata hivyo, kuna barabara nyingi katika jimbo langu ambazo ni muhimu na haziridhishi hata kidogo kwa matumizi ya wakaazi wa maeneo hayo ikiwemo barabara ya Mchangamdogo-Kinyikani- Mzambarau Takao.

(a) Je, unakumbuka ni mara ngapi barabara hii imewahi kupimwa na kuwekwa alama (bench mark) kwa ajili ya ujenzi.

(b) Katika mpango wa ujenzi wa barabara za vijijini ambao kwa bajeti ya mwaka huu Serikali imepanga kujenga kilomita 200 kwa kiwango cha lami. Je, barabara hii itanufaika na mpango huu ukizingatia kuwa ni kongwe na imeshawekewa ahadi nyingi na viongozi waliotangulia.

(c) Je, unawaahidi nini wakaazi wa maeneo hayo katika ujenzi wa barabara hii.

48. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani)
Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Wananchi wanazidi kuishukuru Serikali kwa ujenzi wa barabara inayotoka Mzambarauni hadi Finya kupitia Mchangani. Hata hivyo, ujenzi wa barabara hiyo umewacha viungo ambavyo vinaweza kuhatarisha maisha ya watumiaji na wapita njia zinazoingia ndani kutoka barabara kuu hiyo hasa katika kiunganishi kinachoingia katika kijiji cha Mchangani.

(a) Je, ni lini Serikali itasawazisha viunganishi hivyo vinavyoingia kwenye vijiji vilivyomo ndani ya Jimbo la Pandani kikiwemo kiungo kinachoingia katika kijiji cha Mchangani.

(b) Je, ni hatua ipi iliyobaki inayohitaji kukamilishwa na Mkandarasi ili Serikali pamoja na wadau wengine waweze kuridhia ukamilifu wa barabara hiyo.

**Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:**

26. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Pamoja na kuwepo kwa maelekezo mazuri na ratiba ya mwaka ya masomo katika skuli za Zanzibar, imekuwa ni jambo la kawaida sasa kwa skuli takriban zote za Zanzibar kuendesha masomo ya ziada ya kulipia na kambi za kulipia zisizo rasmi kwa wanafunzi wanaokaribia kutahiniwa katika ngazi za darasa la nne, darasa la sita, kidato cha pili, kidato cha nne na kidato cha sita. Hali hii imekuwa ikiharibu mipango ya wazee hasa katika bajeti za elimu za watoto wao.

(a) Je, Serikali inatambua na kubariki kuwepo kwa mipango hii katika skuli za Serikali na binafsi.

(b) Je, Serikali haioni haja ya kupunguza ukubwa wa mitaala wa madarasa hayo ili skuli zisiwe na sababu ya kuwa na masomo ya ziada na kambi zisizo rasmi.

(c) Je, ni lini Serikali itapiga marufuku au kurasimisha masomo ya ziada ya kulipia na kambi za kulipia ili skuli zote zifuate ratiba kuu ya Serikali ya mwaka.

127. MHESHIMIWA FATMA RAMADHAN MOHAMMED (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Katika Mkoa wa Mjini Magharibi kuna skuli moja tu ya watoto wenye ulemavu wa masikio iliyopo Mwanakwerekwe. Jambo hili linapelekea usumbufu kwa watoto hao, kwani wapo wanaoishi mbali sana na kupelekea baadhi ya wanafunzi kushindwa kabisa kuendelea na masomo.

Je, Wizara imejipanga vipi kuwasaidia watoto hao angalau kila Wilaya kuipatia skuli moja.

**Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:**

34. MHESHIMIWA KOMBO MWINYI SHEHE (Jimbo la Wingwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Serikali imeanzisha utaratibu wa kuyakodisha mashamba ya Serikali ama eka kwa watu tofauti tofauti kila msimu wa karafuu unapofika.

(a) Je, ni kiasi gani cha fedha zinazopatikana ndani ya Serikali kupitia mashamba hayo ya mikarafuu yanayokodishwa kwa kipindi cha miaka ya 2019 na 2020.

(b) Je, Serikali ina uhakika gani kuwa hayo mashamba wanayoyakodisha kuwa yote ni ya Serikali na wanayajua na mipaka yake.

**<u>Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto:</u>**

229. MHESHIMIWA MWANAJUMA KASSIM MAKAME (Nafasi ya Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto:

Tunaipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuwaweka waratibu wa shughuli za wanawake katika kila Wilaya za Unguja na Pemba, waratibu ambao kazi yao kubwa ni kushughulikia kesi za udhalilishaji wa wanawake na watoto na kwa kiasi kikubwa waratibu hawa wamefanikiwa kuisaidia Serikali juu ya hili.

Je, Serikali imejipanga vipi katika kuwasaidia waratibu hawa kwa kuwapatia ajira za kudumu hasa tukizingatia wameshatumikia Serikali yao kwa kipindi kirefu.

232. MHESHIMIWA HAMZA HASSAN JUMA (Jimbo la Shaurimoyo) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto:

Kwa zaidi ya mwezi mmoja sasa tokea mwezi Oktoba 2021, kumekuwa na upungufu mkubwa wa gesi katika Hospital yetu ya Rufaa ya Mnazi Mmoja na wananchi wengi wamekuwa wanalalamika hasa wakati wa operation.

(a) Je, uhaba huu umetokana na kitu gani.

(b) Kwa kuwa hivi sasa dunia ikiwemo Zanzibar imekumbwa na janga la maradhi ya Corona na moja kati ya tiba ya gonjwa hili ni matumizi ya gesi. Je, hatuoni ukosefu wa gesi kwenye hospital hiyo ni kupelekea vifo kwa watu wetu ambapo kama gesi ingelikuwepo wangeliepuka vifo hivyo.

(c) Je Serikali ina mkakati gani katika kutatua tatizo hilo la ukosefu wa gesi.

**<u>Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda:</u>**

99. MHESHIMIWA SHAMATA SHAAME KHAMIS (Jimbo la Micheweni) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda:

Kumekuwa na malalamiko mengi kwa wafanyabiashara wadogo wadogo hapa Zanzibar, kulalamikia juu ya wingi wa taasisi za kutoza kodi kwa wafanyabiashara (utitiri) na pia bidhaa iliyosafirishwa kutoka Unguja kwenda kulipiwa “ofeji” na malalamiko mengineyo kwa pande zote za bandari na kupelekea bei kupanda na kusababisha mzigo wa gharama kwa watumiaji (wateja).

(a) Je, Serikali inafahamu malalamiko hayo ni miongoni mwa sababu zinazopelekea wafanyabiashara kushindwa kuzishusha bei bidhaa zao na kuendelea kuwaumiza wananchi wetu.

(b) Je, ni lini Serikali itaziunganisha kodi na kuondoa au kupunguza viwango vyake ili wafanyabiashara wapate unafuu wa kuwasaidia wananchi wenzao.

(c) Je, Serikali inatoa kauli gani kwa wafanyabiashara hasa wanaosafirisha bidhaa kutoka bandari za Unguja na bandari za Pemba juu ya ulipiaji wa gharama zinazofanana.

**<u>Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale:</u>**

105. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale:

(a) Je, ni maeneo gani ya kihistoria na mambo ya kale ambayo ni vivutio muhimu vya utalii yamevamiwa na watu au taasisi binafsi na kwa kiasi gani yanainyima Serikali mapato.

(b) Je, Wizara ina mikakati gani ya kiuhalisia na isiyo ya udanganyifu ya kuyarejesha maeneo hayo kwenye mikono ya Serikali ili kuweza kuiongezea mapato ya fedha za ndani na za kigeni.

**Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi:**

217. MHESHIMIWA SULUBU KIDONGO AMOUR (Jimbo la Mkwajuni) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi:

Serikali imekataza baadhi ya zana za uvuvi kama mshare, umangu na uchokoo ambazo wananchi wengi hutumia kwa ajili ya kujipatia mahitaji yao ya vyakula vya kila siku. Hata hivyo, wavuvi wamekabiliwa na tatizo la kukamatwa na kupelekwa vituo vya polisi na hatimae hutolewa kwa kulipishwa fidia kutokana na makosa hayo.

Je, ni lini Serikali itatoa ruhusa ya kutumiwa kwa zana mbadala za uvuvi ili wananchi waache kutumia zana zilizokatazwa, ukizingatia wananchi wengi wanategemea kupata vyejio vyao kupitia shughuli za uvuvi.

**Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:**

54. MHESHIMIWA ABDALLA ABASS WADI (Jimbo la Nungwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:

Naipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa juhudi zake kubwa inazozichukuwa kwa ajili ya kutatua migogoro ya ardhi ndani na nje ya nchi yetu ikiwemo jimbo la Nungwi.

Je, ni ipi juhudi ya kutatua migogoro ya viwanja vilivyouzwa kwa zaidi ya watu wawili.

## IV. TAARIFA YA SERIKALI:

**Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:**

Taarifa ya Serikali kuhusu Ripoti ya Hali ya Mazingira Zanzibar.

## V. HOJA ZA MJUMBE:

**Mheshimiwa Hudhaima Mbarak Tahir:**

Hoja ya Mjumbe Kuhusu kuanzishwa kwa Jumuiya ya Wawakilishi kuhusiana na Idadi ya watu na Maendeleo Zanzibar.

**Zanzibar,**
**21 Disemba, 2021.**

**(Raya Issa Msellem)**
**KATIBU WA BARAZA.**